

Barua taka

Kwa kila tukio, tambua iwapo ujumbe ni barua taka na iwapo unafaa kushiriki maelezo na mtu. Tafadhali andika majibu yako kwa kila swali kwenye nafasi uliyopewa.

Tukio la 1

Unapokea barua pepe kutoka kwa wakili, inayokueleza kuwa jamaa wa mbali amekutaja kama mfaidi kwa jumla ya pesa. Inasoma, "Ili kupokea pesa, tafadhali nitumie nambari yako ya akaunti ya benki na nambari ya uelekezaji, ili tuweze kukamilisha uwekaji pesa kwenye benki."

Tukio la 2

Rafiki anakutumia matini, inayokufahamisha kuwa anajaribu kuangalia picha uliyomwonyesha awali lakini hanaa kibali cha kuiona. Huwezi kufikia kompyuta yako kwa sasa ili kumtumia picha. Anajibu, "Ninaweza kuingia kwenye akaunti yako haraka zaidi ili kupakua picha — nenosiri lako ni lipi?"

Tukio la 3

Unapata barua pepe iliyoelekezwa kwako kutoka kwa shule yako, inayodai kuwa akaunti nyingi za wanafunzi zimelaghaiwa. Wanadai, "Hivi karibuni tumetambua kuwa akaunti nyingi za wanafunzi zimeathiriwa. Tunaomba msamaha na tunashughulika ili kurekebisha tatizo. Ili kuweka upya akaunti yako, tafadhali jibu kwa barua pepe hii na jina lako la mtumiaji na nenosiri."

Tukio la 4

Unapokea barua pepe kutoka kwenye benki yako ambapo una akaunti halali. Barua pepe inasema kuwa wamelaghai na kuwa unafaa kuingia ili kubadilisha nenosiri la akaunti yako haraka iwezekanavyo na mabadiliko ya nenosiri kwenye akaunti zozote zinazoshiriki nenosiri hilo.

Barua taka: Nakala ya Mwalimu

Kwa kila tukio, tambua iwapo ujumbe ni barua taka na iwapo unafaa kushiriki maelezo na mtu. Tafadhali andika majibu yako kwa kila swali kwenye nafasi uliyopewa.

Tukio la 1

Unapokea barua pepe kutoka kwa wakili, inayokueleza kuwa jamaa wa mbali amekutaja kama mfaidi kwa jumla ya pesa. Inasoma, "Ili kupokea pesa, tafadhali nitumie nambari yako ya akaunti ya benki na nambari ya uelekezaji ili tuweze kukamilisha uwekaji pesa kwenye benki."

Kuna uwezekano mkubwa barua pepe hii ni barua taka. Hata iwapo ni sahihi tumia jina laa jamaa yako, anaweza kuwa sio anayedaiwa. Huenda mtumaji amepata maelezo kuhusu uhusiano wenyu kupitia mbinu zingine. Kushiriki maelezo yako ya akaunti ya benki kila mara ni hatari na inafaa kufanyika kwa uangalifu. Usiwahi kamwe kutuma maelezo yako kwa mtu isipokuwa umewasiliana na yeye kwanza, na hata baada ya hapo kuwa makini zaidi. Kwa mfano, inaweza kutokuwa hoja nzuri kutuma maelezo yako kupitia barua pepe kwa kuwa haijasimbwa fiche. Ndio maana hospitali nyingi, mawakili, na benki zina tovuti maalum ya kuwasiliana na wewe.

Tukio la 2

Rafiki anakutumia ujumbe wa maandishi, unaokufahamisha kuwa anajaribu kuangalia picha uliyomwonyesha awali lakini hana kibali cha kuiona. Huwezi kufikia kompyuta yako kwa sasa ili kumtumia picha. Anajibu, "Ninaweza kuingia kwenye akaunti yako haraka zaidi ili kupakua picha — nenosiri lako ni lipi?"

Wakati hii sio barua taka, unafaa kutoshiriki manenosiri yako na watu wengine. Pindi wanapopata nenosiri lako, wanaweza kukufungia nje ya akaunti yako au kufikia akaunti zingine za mtandaoni kwa nenosiri sawa. Kwa kuongezea, iwapo mshirika mwingine, mlaghai au mtazamaji ataona ujumbe wako, watu zaidi wanaweza kufikia akaunti yako bila wewe kujua.

Tukio la 3

Unapata barua pepe iliyoelekezwa kwako kutoka kwa shule yako, inayodai kuwa akaunti mingi za wanafunzi zimelaghaiwa. Wanadai, "Hivi karibuni tumetambua kuwa akaunti nyingi za wanafunzi zimeathiriwa. Tunaomba msamaha na tunashughulika ili kurekebisha tatizo. Ili kuweka upya akaunti yako, tafadhali jibu kwa barua pepe hii na jina lako la mtumiaji na nenosiri."

Ni mazoea ya kawaida kutoomba watumiaji maelezo haya. Hata iwapo mtumaji anaonekana kuwa halali, unafaa kuchukulia kuwa barua pepe yoyote inayoomba nenosiri lako ni barua taka.

Tukio la 4

Unapokea barua pepe kutoka kwenye benki yako ambapo una akaunti halali. Barua pepe inasema kuwa wamelaghai na kuwa unafaa kuingia ili kubadilisha nenosiri la akaunti yako haraka iwezekanavyo na mabadiliko ya nenosiri kwenye akaunti zozote zinazoshiriki nenosiri hilo.

Mwendo mzuri wa hatua ni kufungua kidirisha cha kivinjari kipya na kufikia tovuti kama vile ungefikia kwa kawaida. Ufichuzi wa aina hii (kuwa akaunti zimelaghaiwa) kwa kawaida utatajwa kwenye kampuni au kituo cha mteja wa benki. Maagizo kuhusu kituo yanafaa kuweza kufuatwa kwa usalama. Kama katika Tukio la 3, hakuna mhusika halali ataomba stakabadhi za akaunti kutoka kwa kwako kwenye barua pepe.